

جمعية الدعوة والإرشاد وتنمية المجالس بالزلفي
مشروع تَعْلُم الإسلام – أصول العقيدة - سواحيلي

Samo la 9

الدرس التاسع

MAANA YA KUSHUHUDIA KUWA MUHAMMAD NI MJUMBE WAKE ALLAH (SW).

Maana yake ni kutambua kwa dhahiri na kwa ndani ya kwamba Muhammad (saw) ni mja wake Allah na mtume wake, amemtuma kwa ajili ya watu wote, na kwa kulifanyia kazi hili, ni kumtii mtume kwa yale yote anayo amrisha, na kumsadikisha yale anayo yaeleza na kujiepusha na yale yote anayoyakataza na kuyakemea na kusiabudiwe chochote ila kile ambacho kipo kwenye sharia ya Allah.

Na kushuhudia ya kuwa Muhammad ni Mtume wake Allah, kuna nguzo mbili muhimu ambazo ni;

- Nguzo ya kwanza ni Muhammad ni mja wa Allah na Mtume wake, nguzo hii inakataza kuchupa mipaka katika haki yake Mtume kuwa yeye ni mja wa Allah na mtume wake, na yeye Muhammad (saw) ni kiumbe aliyekamilika na hizi sifa mbili alizokuwa nazo.

Kwani maana ya kuwa ni mja wa Allah, kuwa yeye ni mja mwenye kumilikiwa, kwa hiyo ni mwanadamu aliyeumbwa mionganoni mwa viumbe vyake Allah (sw), yanampata kama vile yanayo wapata wengine katika viumbe.

قال تعالى: ﴿ قُلْ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ ... ﴾ [الكهف: ١١٠]

Allah (sw) anasema : (" Sema uwaambie kuwa, hakika sivinginevyo mimi ni mwanadamu mfano wenu") (Al- kahfi :110).

Allah (sw) anasema :

وقال سبحانه: ﴿ الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَنْزَلَ عَلَى عَبْدِهِ الْكِتَابَ وَمَنْ يَجْعَلْ لَهُ عِوْجَأً ﴾ [الكهف: ١].

(" Kila sifa njema ni zake Allah ambae amemteremshia mja wake kitabu asikifanye ni chenye kupotoka") (Al-Kahf: 1).

- Nguzo ya pili ni kujua maana ya Rasuul (mjumbe wa Allah), maana yake ni aliyetumwa kwa watu wote kwa ajili ya kulingania kwa ajili ya Allah , kuwabashiria watu mambo ya kheri na kuwaonya watu na mambo ya shari, na katika kushuhudilia hili katika hizi sifa mbili ambazo ni kukataa kuchupa mipaka katika haki ya bwana mtume (saw), kwani wako wengi katika wafuasi wake wanaochupa mipaka katika haki ya mtume na wakampandisha katika daraja ya juu Zaidi, kwa kumtoa katika nafasi yake yake ya utume na kumpandisha katika nafasi ya kuabudiwa kinyume ya Allah (sw), wakamtaka msaada kinyume ya Allah, wakamta awafanyie mambo asiyokuwa na uwezo nayo isipokuwa Allah pekee katika kuwakidhia haja zao, na kuwaondolea matatizo yao, na wako wengine ambao walipinga ujumbe aliokuja nao mtume (saw).

Wako ambao walimuata mtume na kumtweza katika haki yake ya wajibu, wakayatanguliza maneno ya waja Zaidi kuliko maneno ya Mtume (saw), wakapuuza sunnah za mtume (saw) na wakategemea maneno yanayo kwenda kinyume na aliyokuja nayo mtume (saw).